

Toleo la. 14

Jarida la *Ni Magufuli Tena*

2020 - 2025

ALIAHIDI | AMETEKELEZA | APEWE TENA 5 | 13 SEPTEMBER, 2020



MACHO YOTE CHATO...!



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**

TAHARIRI

HOJA YA MAENDELEO YA WATU NA VITU NI MUFLISI

Baadhi ya viongozi wa vyama pinzani wamekuwa wakiwahadaa wananchi kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya Dkt John Pombe Magufuli, imeleta maendeleo ya vitu na si ya watu.

Mjadala huu tunasema ni muflisi kwa sababu hauna mantiki yoyote katika uhalisia. Hakuna maendeleo yanayohusu watu bila kuweka miundombinu muhimu ambayo ni vitu.

Hii ya vitu na watu ni nahau tamu isiyo na maana yoyote na hata matukio ya viongozi wenyewe wa upinzani kuonekana kupita kwenye barabara zile zile, madaraja yale yale wanayoyaponda na hata kupanda ndege zile zile wanazoponda au kutumia viwanja vya ndege wanavyovipinga, wanapopita kwenda Ulaya, ni ushahidi kuwa nahau hii sasa imezikwa rasmi.

Imezikwa rasmi kwa sababu hata wapinzani wenyewe sasa wanaonekana kuiasi na kila siku wanatumia "vitu" hivyo hivyo kujipatia "maendeleo" yao kwa kuwezesha kufanya shughuli zao za siasa.

Tumemuona Tundu Lissu amerejea nchini na kupita kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Terminal III, Dar es Salaam. Akashangaa shangaa na kufurahia uwanja ule.

Juzi tu mgombea wa ACT ametokomea ughaibuni akipita kwenye uwanja huohuo ambao ni "kitu" kilichomsaidia kwenda nje.

Zitto Kabwe amesema sana kuwa ndege si maendeleo, sasa ghafla juzi hakupanda mawese kwenda kwao Kigoma bali kapanda Bombardier.

Ndio maana sisi tunaendelea kusesitiza kuwa Serikali yetu isisite kuendelea kuwekeza na kujenga miundombinu kwani kwa sasa mjadala wa dhana potofu ya watu na vitu umefungwa rasmi.





MAGUFULI KUUNGURUMA CHATO

Na Mwandishi Mahususi - **CHATO**

Wakazi wa Wilaya ya Chato, Mkoani Geita wamesema wanamsubiri kwa hamu kumsikiliza Mgombea wa Urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM), Rais Dkt. John Pombe Magufuli ambaye anatarajia kuwahutubia wananchi wa wilaya hiyo katika Uwanja wa Mazinati na kuomba kura ili aiongoze tena Tanzania kwa mafanikio kwa miaka mingine mitano.

Wakizungumza na Jarida hili kwa nyakati tofauti leo, wakazi wa Chato wamesema kuwa wataidhihirishia dunia kwamba mcheza kwao hutunzwa kutokana na Rais huyo kuibadilisha Tanzania kuwa yenye maendeleo pamoja na wilaya ya Chato ambayo imekuwa mji mkubwa.

Mmoja wa wakazi wa wilaya hiyo, Elikana Songoma, anasema yeye na familia yake watajitokeza na kuhamasisha wananchi wengine kujitokeza kumsikiliza katika kampeni na watahakikisha wanampa kura ya ndio.

"Mbali na kuleta maendeleo ya Taifa zima, Rais Magufuli ameijenga Chato na kuitangaza duniani, Rais wa Kenya na Uganda wamekua wakifikia hapa kwa sababu tuna uwanja wa ndege," anaeleza Songoma.

Nae Sebastian Maguha amesema wakazi wa Chato wamenufaika sana na huduma za kijamii zilizoboreshwa na Serikali ya Awamu ya Tano hivyo fadhila pekee kwa Rais Magufuli nikujiitokeza kwa wingi kumsikiliza na kuhakikisha anapigiwa kura zote za ndio.

"Tuna vituo vya afya, shule, viwanda, barabara za kisasa zenye taa, umeme, kwa kweli Magufuli ametuthamini sana. Tutajitokeza wote kumsikiliza na tutahakikisha wapinzani hawapati hata kura moja" ameeleza.



MAGUFULI KUIPAISHA SEKTA YA UVUVI

Na Mwandishi Wetu

Mgombea Urais wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli atawainua wavuvi nchini katika kipindi cha miaka mitano ijayo kwa kuweka miundombinu yatakayowezesha kuongeza uzalishaji wa samaki kutoka tani 16,000 hadi 50,000 kwa mwaka na kupanua wigo wa ajira kwa vijana ili kukuza uchumi.

Kupitia Ilani ya CCM ya mwaka 2020-2025, Serikali ya Awamu ya Tano imepanga kununua meli tano za uvuvi zenye uwezo wa kuvua samaki bahari kuu hivyo kuongeza ajira zaidi ya 15,000 kwa mwaka na kuboresha maisha ya wavuvi na wananchi kwa ujumla.

“Tutajenga bandari ya uvuvi katika ukanda wa Pwani ambayo itawezesha meli za uvuvi kutia nanga kwa lengo la kuhaulisha na kuuza samaki, kutoa takwimu sahihi na huduma nyingine. Katika hatua hii Serikali ya CCM inatarajiwa kuzalisha takriban ajira 30,000 na kuongeza pato kwa jamii”, Inasisitiza sehemu ya Ilani hiyo.

Sambamba na hilo, Rais Dkt. Magufuli anasisitiza kupitia ilani ya CCM, kuanzisha na kuimarisha vikundi na Vyama vya Ushirika vya Msingi vya Wavuvi Wadogowadogo ili kuwapatia mitaji, ujuzi, vifaa pamoja na zana za uvuvi katika maeneo ya mwambao wa Bahari ya Hindi, Maziwa, mabwawa na mito ili kuongeza uzalishaji, ajira na kukuza kipato.

“Serikali itatekeleza mikakati ya kuwezesha viwanda vilivyopo kuwa shindani na kuhamasisha mashirika ya umma na sekta binafsi kuwekeza katika uanzishwaji wa viwanda saba vipya vya kusindika na kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi”, inasisitiza Ilani.

Pamoja na hilo, CCM inasisitiza kuwa Serikali itapitia upya tozo katika maeneo mbalimbali ili kuwapunguzia wavuvi kero na kuvutia wawekezaji.



RAIS MUSEVENI AMTAKIA MAGUFULI USHINDI WA KISHINDO

Na Mwandishi Wetu - **Chato - GEITA**

Rais wa Uganda, Mhe. Yoweri Kaguta Museveni ameguswa na uongozi wa Rais Dkt. John Pombe Magufuli na hivyo kumtakia ushindi katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, 2020 ili aiongoze tena Tanzania kwa kipindi cha miaka mitano-jayo.

Mhe. Museveni ametakia ushindi Rais Magufuli leo mjini Chato alipozungumzia hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Hoima Uganda hadi Chongoleani mkoani Tanga.

“Namshukuru Rais Magufuli kwa kunialika hapa Chato leo siku ya Jumapili. Najua yeye na wagombea wa Chama Cha Mapinduzi wanatafuta kura hivyo nawaomba kwa Mungu wapate ushindi”, ameeleza Rais Museveni.

Aidha, Rais Museveni ameahidi kurejea nchini kwa mazungumzo na Rais Magufuli kuhusu namna Uganda inavyoweza kununua gesi inayopatikana kwa wingi Tanzania.

Aidha, Rais Museveni ameonesha kuguswa na namna CCM inavyoongozwa kisayansi na Rais Magufuli na kueleza kuwa atakaporejea tena nchini Tanzania ataomba fursa ya kukutana na kufanya kazungumzo na wanachama wa Chama hicho.



MAGUFULI KURAHISISHA UPATIKANAJI WA PEMBEJEO KWA BEI NAFUU

Na Mwandishi Wetu - **NDANDA**

Mgombea Mwenza wa Urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) ambaye pia ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan amesema Serikali ya CCM inayoongozwa na Dkt. John Pombe Magufuli, imepanga kununua pembejeo za kilimo na kuvipa Vyama vya Ushirika ambavyo vitawauzia wakulima kwa bei nafuu ili kuimarisha kilimo nchini.

Samia aliyasema hayo leo wakati akihutubia mkutano wa Kampeni uliofanayika katika viwanja vya Madeko katika Jimbo la Ndanda, Wilayani Masasi, Mkoa wa Mtwara na kufafanua kwamba mpango huo unaotarajia kuanza katika msimu ujao wa kilimo pamoja na kuwanufaisha wakulima pia unalenga kuzalisha mazao bora yenye tija katika soko la kimataifa.

"Kuhusu changamoto ya upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa wakati na kwa gharama nafuu, Serikali ya Awamu ya

Tano chini ya uongozi madhubuti wa Dkt. John Pombe Magufuli tumepanga kununua pembejeo zote kwa pamoja kupitia Vyama vya Ushirika ambavyo vitawauzia wakulima. Tunataka kuwainua wakulima," alisema Samia.

Akizungumza madai ya fedha za wakulima amesema mapema mwaka huu Serikali ilitoa pesa kuwalipa wakulima wa zao la korosho kupitia Chama cha Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS) lakini baadhi ya viongozi wa Chama hicho wamekuwa sio waaminifu kwani wamekopa fedha hizo hatua iliyosababisha kuwacheleweshea wakulima pesa zao.

"Ndugu zangu wa Masasi, Serikali ilitoa fedha kwa wakulima wa zao la korosho wanaodai fedha zao, lakini kuna baadhi ya viongozi wa AMCOS wamekopa fedha hizo, nawapa mwezi mmoja kuzirudisha, naagiza wakuu wa mikoa na wilaya kusi-mamia malipo haya kwa wakati, "amesema Samia".



MHE. SAMIA AWAHAKIKISHIA USALAMA WA TANZANIA SIKU YA KUPIGA KURA

• Awaonya Wanajiandaa Kuleta Vurugu

Na Mwandishi Wetu - **MASASI**

Mgombea Mwenza wa Urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) Mhe. Samia Suluhu Hassan amesema Serikali itahakikisha inasimamia zoezi zima la uchaguzi na kwamba utakuwa huru na haki na hakuna mtu yeyote atakaeathirika siku hiyo na kuwataka watu wanaopanga kufanya fujo kuacha mipango yao hiyo.

Mhe. Samia amesema amani na utulivu uliokuwepo kwenye chaguzi zilizopita ndivyo itakavyokuwa kwenye Uchaguzi Mkuu unaotarajia kufanyika Oktoba 28, 2020.

Ameyasema hayo kufuatia Mgombea wa Ubunge wa Jimbo la Masasi Mjini Bw. Geoffrey Mwambe kumwambia kuwa kuna Mgombea mmoja wa Ubunge wa chama pinzani kwenye Jimbo hilo ametangaza kufanya fujo siku ya kupiga kura.

"Niwahakikishie watu wa Masasi, Mtwara kuwa Serikali ya CCM itamlinda kila mwananchi katika zoezi zima la upigaji kura kama ambavyo inawalinda siku zote, nendeni mka-pige kura na hakuna hata mbu atakaewang'ata," alisema akiashiria kuwa hakuna mtu atakayedhuriwa.

Alisema CCM ni Chama cha amani na utulivu na kuwataka wakazi hao kumchagua Dkt John Pombe Magufuli ili aendelee amani sambamba na kuijenga nchi.

"Mchagueni Dkt John Pombe Magufuli, yeye ndie Kiongozi imara, mpenda maendeleo na mwenye kuimarisha amani ya nchi, msifanye makosa," alieleza Mhe. Samia.

5 KALI ZA CHAMA CHA MAPINDUZI

Sekta ya Uvuvi

01

Kodi katika zana na malighafi za uvuvi zikiwemo injini za kupachika, nyuzi za kushonea nyavu na vi fungashio ziliondolewa katika kipindi cha mwaka 2015/2020 ili kuwawezesha wauvuvi katika kazi zao.

02

Katika kipindi cha mwaka 2015 - 2020, Serikali ilihamasisha ufugaji wa samaki katika maeneo yenye ukame nchini kutoka mabwawa 153 mwaka 2015 hadi mabwawa 445 mwaka 2020, yamechimbwa katika mikoa ya Dodoma, Singida, Shinyanga, Simiyu, Tabora pamoja na vizimba 7 katika bwawa la Mwamapuli Tabora.

03

Katika Ilani ya CCM ya Mwaka 2020/2025, Serikali itaweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa vi faa bora vya uvuvi, kuzuia uzalishaji na uagizaji wa zana haramu za uvuvi na kuhamasisha uwekezaji katika uzalishaji wa vyakula vya samaki.

04

Serikali itaimarisha miundombinu ya uvuvi kwa kujenga mialo tisa katika maeneo ya Ziwa Victoria (3), Ziwa Tanganyika (4), Nyasa (2) na kuimarisha masoko ya samaki ya Feri Dar es Salaam, Kirumba Mwanza, Kipumbwi Pangani, Sahare Tanga ili kuongeza thamani.

05

Serikali ya Chama cha Mapinduzi itahakikisha sekta ya uvuvi inaimarika kwa kuongeza matumizi ya sayansi na teknolojia ya uvuvi endelevu ili kuhimili ushindani na kufanya nchi kujitosheleza kwa mahitaji ya samaki na kuacha kuagiza samaki kutoka nje.



TUTAANZISHA MAMLAKA YA MAJI CHEMBA - MAJALIWA

Na Mwandishi Maalum - RUVUMA

Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa amesema Serikali inapanga kuanzisha Mamlaka ya Maji Chemba hivi karibuni.

Ametoa kauli hiyo leo wakati akizungumza na wananchi katika eneo la Mnadani, Kijiji cha Kelema, Kata ya Paranga, wilaya ya Chemba mkoani Dodoma kwenye mkutano wa kumuomba kura Rais Dkt. John Pombe Magufuli na mgombea Ubunge jimbo la Chemba, Mohammed Moni na wagombea udiwani wa CCM.

Amesema Serikali itaanzisha Mamlaka ya Maji katika wilaya hiyo na kwamba Serikali ilitoa shilingi bilioni 1.688 za kutafuta vyanzo vya maji huko Orada, Kisanga, Moi, Mondo na Ndaki. "Pia Serikali ya Awamu ya Tano imetoa shilingi milioni 677 za kuchimba visima huko Mondo, Mrijo Juu, Chamba-lo, Hamai na Chemba.

"Tuna uhakika tukipata lita za maji za ujazo 4,700 zingatoshwa kabisa kujenga mtandao wa maji. Kazi ya kuboresha miundombinu ya maji inaendelea. Zimetengwa fedha nyingine, shilingi milioni 150 za kusambaza maji Kelema, Msaada na Bumbu," alisisitiza.

Katika Sekta ya Afya, Mhe. Majaliwa amesema zimetolewa shilingi bilioni 1.8 za kujenga hospitali ya wilaya ya Chemba. "Nia yetu ni kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma hukohuko aliko kwa kuweka zah-anati katika kila kijiji, vituo vya afya kwa kila kata. Wakimaliza ujenzi, tumetenga shilingi milioni 500 za vifaa vya hospitali kwa majengo yote saba."

"Tumepeleka shilingi milioni 400 za kituo cha afya kule Hamai, shilingi milioni 500 kule Mrijo na shilingi milioni 400 kule Kwa Mtoro. Kazi ya ujenzi ikiisha, kila kimoja kitapata shilini milioni 250 za vifaa vya tiba. Ninawaomba mumpye kura Rais Dkt Magufuli, Mbunge na madiwani wa CCM ili tukamilishe kazi hizi kwa sababu Serikali hii ni ya watekelezaji. Tunasema na tunatenda," alisisitiza Mhe. Majaliwa.

Aidha, Mhe. Majaliwa amesema Rais Magufuli anataka umeme usambazwe kote nchini na ndiyo maana akaamua kupunguza bei ya kuunganisha umeme. "Rais wetu kasema anataka kuona kila nyumba ya mtanzania inawaka umeme. Amepunguza gharama za kuunganisha umeme kutoka shilingi 380,000/- hadi shilingi 27,000/-. Rais wetu kasema ni marufuku kulipia nguzo za umeme," amesisitiza Mhe. Majaliwa.

Jarida la Ni Magufuli Tena

2020 - 2025



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**